

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA MSAJILI WA VYAMA VYA SIASA**

Anwani ya simu: 'SIASA'  
Simu: 026 2137232  
Fax: 026 2136924  
Tovuti: www.orpp.go.tz



Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa  
Viwanja Vya Nanenane Nzuguni  
Jengo la Wizara ya Kazi,  
Mtaa wa Nzuguni A  
P.O. Box 2851  
**DODOMA**

**TAARIFA KWA UMMA**

**KUKARIBISHA MAONI NA MAPENDEKEZO YA KUFANYIWA KAZI NA  
KIKOSI KAZI CHA MHESHIMIWA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA  
TANZANIA**

Natumia fursa hii kuwafahamisha Watanzania wote kuwa, Kikosi Kazi cha Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kinachofanyia kazi masuala yanayohusu Demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa, kinaendelea kupokea maoni na mapendekezo ya wananchi na taasisi mbalimbali katika maeneo yafuatayo:-

<b>Na.</b>	<b>Suala</b>
1.	Mikutano ya hadhara na Mikutano ya ndani ya Vyama vya Siasa
2.	Masuala yanayohusu uchaguzi
3.	Mfumo wa maridhiano ili kudumisha haki, amani, utulivu na Umoja wa kitaifa
4.	Ushiriki wa Wanawake na Makundi Maalumu katika siasa na Demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa
5.	Elimu ya Uraia
6.	Rushwa na Maadili katika siasa na uchaguzi
7.	Ruzuku ya Serikali kwa Vyama vya Siasa
8.	Uhusiano wa Siasa na Mawasiliano kwa Umma
9.	Katiba Mpya

Maoni na mapendekezo yanapokelewa kwa njia zifuatazo:-

1. Barua pepe, taskforcemaoni@orpp.go.tz
2. WhatsApp, ujumbe kwenda kwa Katibu wa Kikosi Kazi, 0784 394883;
3. Barua au nyaraka yoyote kwenda kwa Katibu wa Kikosi Kazi, kupitia Sanduku la Posta 2851 Dodoma; au
4. Kuwasilisha barua au nyaraka husika Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa iliyopo:-
  - i. Dodoma, viwanja vya Nanenane Nzuguni, katika Jengo la Wizara ya Kazi, Mtaa wa Nzuguni A;
  - ii. Dar-es Salaam, mtaa wa Shaaban Robert mkabala na Shule ya Msingi Bunge; au
  - iii. Zanzibar, Mbweni Matrekta.

Vilevile, tarehe 27 Aprili 2022 katika ukumbi wa Adam Sapi Mkwawa wa ofisi ndogo za Bunge zilizopo mtaa wa Shaaban Robert Dar-es salaam, Kikosi Kazi kitaanza kuongea na wadau mbalimbali wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa, kupokea maoni na mapendekezo yao. Ratiba ya kila wiki itakuwa inatolewa kwa umma, ili kuwakumbusha wahusika kuhusu mwaliko wa kuja kuongea na wajumbe wa Kikosi Kazi.

Ratiba ya wiki hii ni ifuatayo:-

Tarehe 27 Aprili, 2022

Na.	Muda	Mtoa Maoni na Mapendekezo
1.	03:00 – 04:00 Asubuhi	Legal and Human Rights Center (LHRC)
2.	05:00 – 06:00 Asubuhi	Jukwaa la Katiba (JUKATA)
3.	07:00 – 08:00 Mchana	Media Council of Tanzania (MCT)

Tarehe 28 Aprili, 2022

Na.	Muda	Mtoa Maoni na Mapendekezo
1.	03:00 – 04:00 Asubuhi	Baraza Kuu la Waislam Tanzania (BAKWATA)
2.	05:00 – 06:00 Asubuhi	Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC)
3.	07:00 – 08:00 Mchana	Kanisa la SABATO Tanzania
4.	09:00 – 10:00 Alasiri	Jumuia ya Wanafunzi Taasisi za Elimu ya Juu Tanzania (TAHLISO)

Tarehe 29 Aprili, 2022

Na.	Muda	Mtoa Maoni na Mapendekezo
1.	03:00 – 04:00 Asubuhi	Baraza Kuu la Jumuiya na Taasisi za Kiislam Tanzania
2.	05:00 – 06:00 Asubuhi	Tanganyika law Society (TLS)
3.	08:30 – 09:30 Mchana	Baraza la Mekanisa ya Kipentekoste Tanzania (CPCT)

Wanahabari mnakaribishwa kupiga picha na kuongea na wahusika kabla na baada ya mazungumzo.

Karibuni sana.



Sisty L. Nyahoza

**KATIBU WA KIKOSI KAZI**

26 Aprili 2022